HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA

ALIYOYASEMA NAIBU WAZIRI, WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI; MHE. ANGELLINE MABULA ALIPOTEMBELEA MANISPAA YA ILALA TAREHE 19 OCTOBA, 2017

- Katika ziara yangu niseme, napita katika Halmashauri zote za Miji, Manispaa pamoja na Jiji kuweza kuzungumza na Watendaji wa Sekta ya Ardhi, lakini pia kuzungumza na Kamati zinazosimamia Sekta ya Ardhi.

- Lengo la ziara yangu, jambo la kwanza ni suala la kukagua mfumo wa kukusanya kodi ya pango la Ardhi katika Halmashauri zetu, lakini vilevile kuangalia mwenendo wa ukusanyaji madeni katika Halmashauri zetu, kwa sababu sehemu kubwa inaonekana kama vile haitiliwi manani sana pamoja na kurahisisha mfumo ambao unawarahisishia kazi zaidi wanaohusika, na hii imejitokeza katika Halmashauri zote hakuna Halmashauri iliyo ‘perfect’ katika mfumo huu kiutendaji.

- Jambo la Pili, ni suala la kuangalia namna ya utendaji kazi wa Mabaraza ya Wilaya, yaani Baraza la Ardhi na Nyumba ambalo linasimamiwa na Wizara, lakini ukiangalia ushirikiano wao na mahusiano yao na Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata ambayo yanasimamiwa moja kwa moja na Halmashauri, kumekuwa na changamoto nyingi kwa hiyo tunakumbushana pale ambapo inabidi kufanya zoezi hilo.

- Kuangalia migogoro iliyopo na namna ambavyo tunaweza kuitatua pale ambapo inatugusa moja kwa moja kama ni Wilaya au Halmashauri basi kujua sehemu yao wamefanyaje katika kuitatua.

- Tupo na wenzetu wa ‘NHC’ ambao ndiyo wamepewa dhamana ya ujenzi wa nyumba za makazi na tunajua Watu wengi hawana nyumba, Watumishi na Watu wengine wa kawaida, lakini pia hata ule uwezo pengine wa Watu kujenga nyumba bado ni wa shida, na wao wanajenga nyumba zikiwa katika ‘category 3’ tofauti, kama zile za gharama nafuu, gharama za kati na za Watu wa hali ya juu, lakini pia wanajenga majengo kwa ajili ya Wawekezaji, lakini kwa Miji ambayo inakuwa, hapa Jiji limeshaukwa limebanana katika pande zote, yaani limekuwa kupita kiasi kwamba huna tena mahali pakupulia, lakini tunazo ‘squatter’ nyingi, tuna ujenzi holela mwingi sasa namna yakuweza kubadilisha uweze kupendeze.

- Lakini wakati huo huo mpo kwenye mchakato wa ‘Master plan’ ambayo mnaiandaa, Je maandalizi yetu yamefikia wapi? na yanakwendaje? Na yameangalia mstakabali wa maeneo yetu yalivyo na namna ambavyo kabla ya kuzindua huo Mpango mtakuwa mmejiandaa ku ‘accommodate’yale maeneo ambayo teyari yapo kwenye zoezi la Urasimishaji. Uzinduzi ukifanyika zoezi la Urasimishaji linakoma, sasa lazimakujenga uelewa wa mazingira ya pamoja. Kwa hiyo tukishaingia kwenye ‘Master plan’ hatutokuwa tena na suala la Urasimishaji’

- Kuna Mheshimiwa amezungumzia Wajumbe ambao wameshapendekezwa lakini Wizara haijateua. Naomba nisilitolee jibu, lakini kuna Magazeti ya Serikali yametoka ‘Session’ hii ya Bunge iliyopita tumepewa, yapo mengi na kuna baadhi ya maeneo ambapo wale Watu wametajwa na Waziri ameshawateua, ila sina hakika kama Ilala ni moja wapo, lakini nitaangalia.

- Eneo la ‘Aviation’ ni eneo la Serikali, lakini pia pamoja na hayo kuna yale masharti ya umiliki kwa kuzingatia lile ni eneo la Serikali na kwasababu Ilala ndiyo mnaosimamia, tunachoweza kufanya ni kuomba kama halitumiki kwa matumizi yao basi lifanyiwe yale matumizi tunaona yanakusudiwa, hiyo ni ‘altenative’ moja wapo, lakini jengine ni kupeleka notisi kwasababu umilikaji wa pale una masharti, sasa kama yale masharti yamekiukwa au yamevunjwa, kwa hiyo angalieni ‘altenative’ zote kwakuomba au kupeleka notisi kwa yale masharti ya uwekezaji wa maeneo.

- Nina Wateja wachache hapa hawafiki hata 50, lakini kwa records za Wizara, kwa Manispaa ya Ilala kodi za ardhi mnazodai kwa Wateja 100 tu, tuliowachukua ambao wana madeni kuanzia Milioni 5, Wateja 100 kati ya viwanja 46,103 sisi tumechukua viwanja 100 tu na katika viwanja hivyo 100 mnadai kodi ya ardhi Shilingi Bilioni 39.854 ‘you can imagine’ pesa ilivyo nyingi nje.

- Agizo langu hapa kwenye suala la makusanyo ni kwamba, kuanzia sasa kila mnapokaa kwenye Kamati ya Mipango Miji lazima Watendaji wawaletee au Mkurugenzi awaletee orodha ya Wadaiwa sugu ambao wame wa ‘save’ notisi katika ‘quarter’ hiyo, ‘quarter’ inayofuata walete ‘feedback’ baada yaku ‘save’ notisi kwenye ‘quarter’ hii wangapi wamelipa kwa hiyari, wangapi wamekaidi wamepelekwa kwenye Baraza la Kata, na watakapopelekwa kwenye Baraza wakiwa wengi, Sisi kama Wizara tunaweza kutoa msaada kwa maana kuwa na wale Mawakili wanaoweza kusimamia makusanyo ya kodi.

- Kama kuna Sekta inayosimamiwa na Wizara 3 tofauti ni Sekta ya Ardhi hasa kwenye migogoro. Migogoro iliyo kwenye ngazi ya chini inasimamiwa na Halmsahauri kwa maana yale Mabaraza yapo chini ya Wizara ya TAMISEMI, waki ‘appeal’ kesi zao kuzipeleka Wilayani ndipo Wizara ina ‘take charge’, wasiporidhika na kukata rufaa kwenda Mahakama Kuu yale tena hayapo Wizara ya Ardhi, anakwenda kwenye Wizara ya Katiba na Sheria, kwa hiyo Wizara ya Ardhi ina mchakato wake katika kupata

ufumbuzi wake, lakini kesi zinakuwa nyingi kwenda juu kwa kuwa hawa waliopo chini tumewapa uhuru mpana wa kufanya maamuzi ambayo hawana uwezo nayo, lakini pia hawana elimu ya kutosha kujua wigo wao mpana kufanya kazi hizi.

Imeandaliwa na:

Kitengo cha Teknolojia ya Habari, na Mawasiliano

Halmashauri ya Manispaa ya Ilala